JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI

Namba za simu;
Mkuu wa Shule +255(0) 717315633
Makamu mkuu wa Shule +255 (0) 678231534
Email. Temekesecondary@yahoo.com

Shule ya Sekondari Temeke
S.L.P 46212
Dar es salaam.
.....

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi;
.....
S.L.P.....
.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NASHULE YA SEKONDARI TEMEKE HALMASHAURI YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA 2020.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka **2021** shule ya Sekondari Temeke ipo umbali wa **Kilometa 3** Kusini Magharibi mwa Wilaya ya **Temeke.**

   USAFIRI WA BASI;
   - Kutoka Mwenge unapanda gari la Temeke Mikoroshini (shuka Maghorofani)
   - Kutoka Kariakoo unapanda gari la Gongolamboto kupitia Nyerere Road (Shuka Tazara)
   - Kutoka Ubungo unapanda gari la Tandika/mbagala kupitia Mandela Road
     (Shuka Tazara)
   - Kutoka Makumbusho unapanda gari la Gongolamboto kupitia Mandela Road
     (Shuka Tazara)
   - Kutoka Mbagala unapanda gari la Gongolamboto, ubungo au Buguruni (Shuka sokoni / Veterinary).

Muhula wa masomo utaanza rasmi tarehe **11/01/2021** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe **11/01/2020** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2020**.

1.0. SARE

1.1. Wavulana

(i) Suruali mbili **(2)** za rangi ya zambarau zisizobana ziwe Inchi **16** kwa chini.

(ii) Mashati mawili **(2)** meupe ya mikono mifupi, yasiyobana, na yasiyo mafupi wala makubwa sana.

(iii) Soksi nyeusi

(iv) Mkanda mweusi wa ngozi usio na urembo

(v) Viatu nyeusi vya ngozi, vya kufunga kamba visivyochongoka mbele na visivyo na marembo.

1.2. Wasichana

(i) Sketi mbili **(2)** ndefu zinazovuka magoti za rangi ya **Zambaru.**

(ii) Mashati mawili **(2)** meupo ya mikono mifupi yasiyobana. Yasiyomafupi wala makubwa sana.

(iii) Soksi nyeupe ndefu

(iv) Wanaovaa hijabu – sketi ziwe ndefu hadi kwenye/ karibu na vifundo vya miguu. Pia zivaliwe na nusu kanzu ambapo kitambaa cha hijabu kifanane na nusu kanzu na kisiwe kitambaa cha mpira. Nusu kanzu ziwe ndefu usawa wa makalio na zisiwekwe zipu. Hijabu iwe ndefu kufunika kifua.

(v) Viatu vyeusi vya ngozi, vya kufunga kamba, visivyochongoka mbele na visivyo na marembo.

N.B: Mavazi yanayoenda kinyume na maelekezo yaliyotajwa hapo juu hayataruhusiwa Shuleni.

1.3. Vifaa binafsi vya mwanafunzi

Mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo'-

- Daftari kubwa zenye kava ngumu (Counterr book) pendekezwa q uire three (12)
- Kalamu za wino (peni)
- Penseli
- Madaftari madogo ya mazoezi **(msomi) 12**
- Mkebe wa hesabu **(mathematical set)**
- Begi la mgongoni lisilo na marembo
- Vitabu vya masomo (wataelekezwa na walimu wao)

N.B. Mzazi anaagizwa kuhakikisha anamnunulia mwanafunzi kamusi itakayokaguliwa – lengo hasa ni kuimarisha uwezo wa lugha kwa mwanafunzi hasa lugha ya kiingereza Dictionary pendekezwa ni **Concise Oxford Dictionary (English iliyotafsiriwa kwa Kiswahili kwa kila mwanafunzi).**

2.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na. 10** ya mwaka **1995.** Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzi ya ufundi, yenye

dhamana ya Elimu chini ya **Ofisi ya Rais (TAMISEMI)** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa.
(d) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzinatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika Shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili. Mavazi na mazingira ya shule.
(f) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa.
(g) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote na
(h) Kutunza mali ya umma.

2.1. makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
v. Kufuga ndevu
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
vii. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi , kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
viii. Uvutaji wa sigara / Bangi
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yote yanayovunja sheria za Nchi.
xii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya Shule.
xv. Kudharau bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama vile; kunywa sumu n.k
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NB. 1. Wasichana wataruhusiwa kusuka kwa kufuata maelekezo watakayopewa na uongozi wa shule.

2. Mwanafunzi akifanya uharibifu au upotevu wa samani za shule kama viti na meza vifaa vya maabara, vitabu n.k. mzazi atawajibika katika kulipa.

3.0. Viambatanisho na fomu muhimu vinavyohitajika virudishwe Shuleni baada ya kujazwa kikamilifu:-

(a) Fomu ya uchunguzi wa afya **(Medical Examination Form)** ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospital ya Serikali.

(b) Fomu ya usajili (Kiambatanisho A)

(c) Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule (Kiambatisho B)

- Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana Temeke Sekondari

.....

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI TEMEKE